SHULE YA UPILI YA WASICHANA YA GATITU S.L.P. 01030 327 GATUNDU

TATHMINI LA MWEZI WA JUNE, KIDATO CHA TATU

Jina.....Nambari ya mtahiniwa .....

Tarehe .....

102/2

KISWAHILI

KARATASI YA 2

LUGHA

MUDA: SAA $2^1/_2$

Maagizo.

*Andika jina lako na nambari ya mtihani katika nafasi zilizoachwa hapo juu.

* Jibu maswali yote. Majibu yote yaandike katika nafasi zilizoachwa wazi katika kijitabu cha maswali.

kwa matumizi ya mtahini pekee

Swali	Mada		
1	UFAHAMU	15	.....
2	UFUPISHO	15	.....
3	MATUMIZI YA LUGHA	40	.....
4	ISIMU JAMII	10	.....
JUMLA		80	.....

1 **UFAHAMU**

(Alama15)

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

Mojawapo ya vipengee muhimu ambavyo mwalimu na mwanafunzi wa isimu jamii anahitaji kujua ni historia ya Kiswahili. Katika kuangazia historia ya lugha hii muhimu ya Afrika mashariki na kati, Mwalimu na mwanafunzi wake hawawezi kukwepa swala la jinsi Kiswahili kimeathiriwa na lugha nyingine.

Utafiti akiolojia au historia chimbo umeonyesha kwamba vyungu vya wachina, maandishi ya wamisri na hata athari za wageni wengine kwa wakazi wa pwani bado zingalipo. Aidha, historia imedokeza kwamba baadhi ya wageni hawa walipiga kambi na kuishi pwani ya Afrika mashariki mapema mwaka 900 baada kristo.

Wageni hao ambao walihamia pwani ya Afrika Mashariki kwa sababu wanazozijua wao wenyewe – waliishi katika eneo hilo na kufunga ndoa na wenyeji wa sehemu hizo. Wanavyosema chirghddin shihabddina,Mathias Mnyapala katika historia ya Kiswahili, wahamiaji hao walichangia katika kupanuka na kukua kwa miji ya mwambao ya waswahili kama vile Pate, Lamu, Vumba, Pemba na Zanzibar. Wajukuu wa waarabu wengi pamoja na waajemi chambilecho Abdala Khalid walisahau lugha zao baada ya muda mrefu na kuanza kutumia Kiswahili. Hali ambapo lugha za baadhi ya wahamiaji hao "zilimezwa" na lugha ya wenyeji wa mwambao kimsingi ilitokana na uchache wao.

Hata hivyo Kiajemi au washirazi kutoka Irani walipokeza Kiswahili maneno mengine ambayo yanapatikana katika lugha hii hadi leo. Himaya ya shirazi na makazi yao kuanzia kisiwa cha Funzi

kusini mwa pwani ya Kenya hadi Tanga na Bagamoyo nchini Tanzania ingali inatambulika ingawa sio kwa njia kinagaubaga hivi leo.

Washirazi walitofautishwa na wakazi wengine wenyeji wa pwani kama vile Wadigo, na Wasegeju kwa sababu ya jinsi walivyoishi maisha yao kijumla. Walitegemea uvuvi na kutumia lahaja ya kipekee ya Kiswahili iliyojulikana kama chichifundi.

Washirazi waliathiri Leksikoni ya Kiswahili katika mianda mbalimbali. Mianda na nyanda hizo ni pamoja na utawala ambapo tunapata maneno kama vile jumbe, diwani, waziri , serikali, shehe, akida, Amiran sultan.

Katika mwanda wa biashara washirazi walichangia maneno kama vile tajiri na bakshishi. Kwenye mwanda wa uchukuzi kwa vyombo vya majini tunapata maneno kama vile bandari, nanga, tezi n.k. Katika taaluma ya mimea washirazi walichangia maneno kama mbangi, Mbilingani, ndengu, Mgulabi, mharagwe, mpopo, mtambwi, mnazi, mdalasini, na derabi. Kuhusu vyakula walichangia ni pamoja na lasi, seredani, utaji, zari, zumari, urujuani, na rangi.

Aidha kwenye taaluma ya ujenzi walichangia maneno kama vile dari, boma, ghala na rosani. Maneno mengine ni bahati, usafidi, huruma, beluwa, hoihoi, ushenzi, barabara, miongoni mwa mengine. Tamthini ya maneno haya inadhihirisha kwamba asilimia tisini ni nomino.
Ni rahisi kwa lugha kukopa nomino kwa sababu kwamba washirazi waliishi na kutangamana kwa urahisi na watu wengine Afrika mashariki, Waswahili walipokea vyema meneno ya lugha yao ambayo mengi yamekumbatiwa na kutumika sana hivi leo. Hii ni ishara kwamba tamaduni za watu hazina budi kuathiriana.

Maswali.

a) Yape makala haya anwani mwafaka. (alama2)

.....

b) Toa ushahidi unaoonyesha kuwepo kwa wageni ambao waliathiri lugha ya kiswahili katika mwambao wa Afrika Mashariki. (alama2)

.....

.....

.....

c) Ni kwa nini waswahili walikubali na kukopa maneno mengi kutoka kwa washirazi. (alama2)

.....

.....

.....

d) Lugha za kigeni ziliathiri lugha ya Kiswahili kwa njia chanya. Eleza. (alama2)

.....

.....

.....

e) Eleza mchango wa washirazi kwa lugha ya Kiswahili. (alama4)

.....

.....

.....

f) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika taarifa . (alama3)

I. Chambilecho. :.....

II. Kinaga ubaga:.....

III. Tamaduni:.....

2. UFUPISHO

(Alama15)

Soma kifungu kifuatacho kasha ujibu maswali.

Ulimwengu wa leo umebadilika ukifananishwa na ule wa zamani. Leo hili jambo likitokea popote ulimwenguni, walimwengu hulipata kwa upesi sana. Hii ni hali ambayo imeathiri namna mabadiliko yanavyotokea na kuivumania jamii yetu. Sasa yeyote anaweza kuivumania jamii yetu.Sasa, yeyote anaweza kupata habari au data aitakayo kupitia mtandao wakati wowote. Shuleni, hali hii imebadilisha nam na ya utoaji mafunzo na masomo kwa jumla. Siku hizi watu wanaweza kufanya maamuzi kwa upesi na kubadilishana mawazo na hivyo kufikia maamuzi hata kupitia kwa barua pepe. Lakini wakereketwa wengine wanadai kuwa hali hii imechangia pakubwa „kuharibika" kwa tabia ya usomaji.

Tukiingia katika starehe au burudani, mambo ni tofauti kabisa hii leo. Hapo zamani, waja walikuwa na njia finyu za kujistarehesha lakini siku hizi ni tumbi nzima. Mwanadamu anaweza kuchagua kujiburudisha akiwa katika chumba cha kulala kupitia mtandao. Hali hii humsaidia mja kustarehe burudani anayoipenda kwa kuwa na uhuru wa kuchagua kutoka miongoni mwa starehe au burudani nyingi. Hata hivyo, kuna shutuma. Hali hii huleta kasumba ya kikoloni kupitia kwa kuiga tamaduni za kigeni hasa lugha na namna ya kuhusiana kimapenzi.

Utandaridhi au utandawazi umezifanya jamii nyingi siku hizi kubadilisha mawazo yao ya utenda kazi wao. Watu wamebadilisha fikira zao kuhusu masuala na dhana potovu, hali ambayo imebadilisha hali ya maisha katika jumuiya. Masuala, mathalani usawa wa kijinsia na mawazo ya kisasa yamekuwa mambo ya kawaida. Watamaduni wanasema kuwa hali hii iliyozuka mwanzoni mwa karne ya ishirini imezorotesha utamaduni wa kiafrika; „kustaarabisha" watu kwa kuchangia kusambaratika kwa kwa familia kutokana na kuongezeka kwa matukio ya kuvunjika kwa ndoa.

Kuwepo kwa utandawazi kumefanya mambo kuwa rahisi kwa njia nyingine. Lakini hali hiyo pia imechangia kuwepo kwa hali ya kuchanganyika hasa miongoni mwa vijana walioweza kuchagua yaliyomema kutokana na yale wanayoyasikia na kuyaona. Baadhi ya watafiti wanasema kuwa, hali hii imechangia kuwepo kwa uvivu miongoni mwa wafanyikazi kwa sababu ya kutazama vipindi runingani kwa muda mwingi. Hili pia limesababisha mabadiliko makubwa katika masomo

kwa vile wanafunzi wengi pia hushiriki katika kujiburudisha kutanzama vipindi katika runinga kwa mfano kipindi cha "Storm over Paradise" ambacho kimekwisha hivi karibuni na kile cha "Tahidi High" Kinachoendelea. Matokeo yamekuwa ni ujanja mwingi miongoni mwa vijana wetu. Hatusemi chochote kuhusu facebook" na kadhalika!

MASWALI

a) Je kuna manufaa yoyote yanayotokana na mabadiliko katika jamii ya sasa? (tumia maneno 40-45) (alama 6, na moja ya utiririko, jumla 7)

Maandalizi

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

Jibu.

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

b) Eleza namna ambavyo hali ya mabadiliko katika jamii imezua matatizo chungu nzima. (maneno 55-60) (alama 7, na moja ya utiririko, jumla 8)

d) Kuna tofauti ipi kati ya mofimu huru na mofimu tengemezi. (alama2)

.....

.....

.....

e) Tungia maneno haya sentensi ukitumia vivumishi virejeshi. (alama2)

(i). Teo.:.....

(ii) Ukuta:.....

f) Unganisha sentensi hizi: (alama2)

Nyumba hii haina vijiko .Nyumba hii haina vikombe.

.....

g) Onyesha matumizi ya kisarufi ya maneno yaliyopigwa mstari. (alama2)

i. Alienda <u>kusoma</u> ng'ambo.

.....

ii. <u>Kusoma</u> kwake kutamfikisha mbali.

.....

h) Yakinisha sentensi ifuatayo. (alama2)

Mbwa hakubweka usiku kucha.

.....

i) Tumia vitenzi vifuatavyo vya silabi moja kutunga sentensi katika hali ya kutendewa. (Alama2)

(i). –fa :.....

(ii). –nywa :.....

j) Kwa kutumia mifano onyesha miundo miwili ya ***kirai – vumishi***. (alama2)

i).....

ii).....

Maandalizi

.....

.....

.....

.....

.....

.....

Jibu

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

3. <u>MATUMIZI YA LUGHA</u>.

a) Tofautisha sauti zifuatazo (Alama40)

/t/:..... (alama2)

/d/

:.....

b) Taja vipashio vinne vya lugha ukianza na kile kidogo zaidi. (alama2)

.....

.....

.....

c) Onyesha kuwa Kiswahili kina miundo ifuatayo ya silabi. (alama2)

i. Silabi Funge

.....

ii. Silabi za konsonanti mbili pamoja na irabu.

.....

k) Andika katika usemi wa taarifa ."Tutakaa hapa kwa muda wa siku kumi" Wageni walisema.

(alama2)

.....

l) Onyesha shamirisho katika sentensi ifuatayo.

Mama alimpa mtoto chai kwa kikombe. (alama3)

.....

.....

m) Andika vinyume vya maneno yaliyopigwa mstari (alama2)

(i). Juma amepiga kilemba.

.....

ii)Fatumaameolewa na salim.

.....

n)Andika sentensi ifuatayo iwe katika hali ya - a - (alama2)

ukarabati wa barabara kuu unaendelea.

.....

o) Onyesha kishazi huru na kishazi tegemezi katika sentensi hii. (alama2)

Mwanasiasa aliyetutembelea jana alitoa ahadi za uongo.

.....

.....

p) Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya matawi . (alama4)

Paka mweusi alikuwa amejificha ndani ya kabati hilo.

.....

.....

.....

.....

.....

.....

q) Taja aina mbili za viwakilishi nafsi. (alama2)

.....

.....

r) Eleza maana mbili zinazojitokeza katika sentensi. (alama2)

Nenda ukaninunulie mbuzi.

i).....

ii).....

s) Liweke neno lifuatalo katika ngeli yake. (alama1)

Kiokote:.....

4.ISIMUJAMII (alama10)

Eleza sifa **tano** za sajili ya maabadini

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....